Kwako bibi

K.H.

Enyi ndumba si mutuache huru !

siku hizi, wakaaji wa jimbo la Kivu kwa jumla na wale wa mji wa Bukavu kwa upekee, wapigwa na bumbuazi kwa kutambua kua akina dada tunaowaita mbaraga (ndumba ao malaya) waanza sasa kuleta mchafuko katika mila ya mababu zetu.

Hapo zamani, mtu alipofariki, jamaa lake pamoja na marafiki ndio waliombwa kufanya vyote wawezavyo kusudi ya kuendesha matanga, ya kumzika na vivi hivi. Lakini kwa leo jambo hilo laanza kubadilika.

Tega sikio nikueleze. Kwa leo, vijana wavulana (garçon) wanapopata habari ya kuwa bibi malaya amefariki, waanza kujitembeza kwa hali ya kitisho. Hawana tena amani. Kwa nini jambo hilo ?

Wamalaya wajipanga katika mabarabara wakiwangoja wapita njia. Kila mtu anayepita njiani aazimishwa kutoa kiasi fulani cha feza eti kitawasaidia kwa kumzika rafiki yao aliyefariki ao kununua vifaa vinavyohitajika kwa kuendesha matanga. Akina dada hao wachukua udongo katika chungu kusudi ya kuwatisha wakaaji wanaopita njiani.

Hapo majuzi walifuata hata ndugu waliojielekeza kunako uwanja Mobutu mtaani Kadutu kusudi ya kuhuzuria kunako mchezo wa kandanda kati ya Bukavu-Dawa na Zaire Bank. Wale wote waliotumbukia katika mtego wao waliazimishwa kulipa zaire kumi. Na yeyote aliyejionyesha kuwa hapendi kulipa hizo feza alipakwa matope kwenyi suruali ao shati yake.

Wamalaya hao hawaelewi kuwa kuna wale jamaa ambao wana hasira kubwa na waweza hata kufikia kuwaonyesha cha mtema kuni. Hata hivyo, usilimu ni kuona wakati wa matanga watu wanaomfahamu marehemu wafika bila kukazwa kumuomboleza kwa kutoa feza, pombe na mashauri kusudi ya kuunga mkono wale waliompoteza marehemu.

Ni hapo ndipo wanatambulika wale wanafiki (hypocrites) wanaofika kumchekelea yule aliyefariki ao ndugu zake.

Tena tunawapasha wadada ndumba kuwa hakuna hata kistari kimoja cha katiba (constitution) ya nchi yetu kinachowaamuru waangamize wakaaji wakiwaomba kwa nguvu wawatolee feza za kuomboleza jamaa la yule aliyefariki.

Goma — Kisha kumnasa "Bwana Tembo"

Mikonga 76 ya tembo imeshikwa kimagendo

Habari zilizoletwa ofisini mwetu na kiongozi wa gazeti JUA pa Goma zaeleza kuwa wachuuzi kimagendo hawana tena haya na woga.

Siku kwa siku, viongozi wa nchi yetu wapiga kelele ya yohe na kulalamika kutokana na kuuawa ovyo kwa wanyama kama vile tembo, ngila, twiga na kazalika.

Tukichukua mfano wa tembo tutatambua wazi kuwa wale wanayo zoezi ya kuwatoa maisha si katika nia ingine bali ni kutaka kuchukua mikonga yao inayo samani kubwa ya feza za kigeni.

Hapo majuzi ni yule jamaa anayejulikana kwa jina la "Bwana Tembo" ndiye aliyetupwa gerezani kisha kuteketeza tembo katika shamba la wanyama la Virunga. Kwa sasa ajuta matendo yake katika jela la hapa mjini Bukavu.

Huko Goma, ni askari jeshi ndio watajwa katika magendo ya kuvusha vifaa kutoka Goma hadi Gisenyi katika jamhuri jirani ya Rwanda. Miongoni mwa vifaa hivyo twaweza kutaja maharagwe, kahawa, na pombe. Bila kusahau magari.

Mnamo siku zilizopita, ofisa mmoja wa ngazi ya "adjudant" alinaswa na pombe ya aina ya "Castel" aliyotaka kuvusha katika gari lake nyeupe la "peugeot 404". Mbele ya hapo mama mmoja naye alivumbuliwa akiwa na sanduku la risasi ya kuua tembo kunako uwanja wa ndege wa kimataifa mjini Goma.

Akida mwengine alivumbuliwa katika njama (complot) ya kutaka kuvusha mikonga (pointes d'ivoire) 76 ya tembo toka Goma hadi Gisenyi (Rwanda). Waliovumbua jambo hilo wasema kuwa byashara hivyo vya magendo vyaweza kufikia samani ya zaire milioni mbili nchini na milioni tano ugenini. Watu wengi hujiuliza ya kuwa mikonga hiyo ni ya mtu gani ao ni nani anayewasukuma askari waivushe hadi nchini Rwanda. Kwani wale wote wanaotajwa hakuna yule anayekubali ya kwamba anaelewa neno kuhusu mikonga hiyo.

Uchunguzi unaofanyika waonyesha wazi kuwa ni vijana wa asili ya kinyarwanda wanaobaki kandokando ya duka la kuuza nyama "La michaudière" ndiyo wanaoendeshwa uchuuzi huo wa magendo.

Jamaa hao wanayo zoezi ya kujikusanya huko Kashebere ambako huchimba zahabu (or) ao katika duka za kimagendo za kuuza zahabu mkoani Virunga.

K.H

JUA

Gazeti la Kivu

Mwaka wa 12 n° 279 — Tarehe 22 mpaka 28 Juni 1985

Kiongozi : Mutiri - wa - Bashara.

Waharamia 7 toka Lybia walionyeshwa kwa wapashaji wahabari



Mareshali Mobutu na askari-jeshi wetu shujaa wawangoja wahuni wowote bila woga.

Kisha kutangazwa kwa habari juu ya vitendo vya uhuni na uharamia vilivyotaka kuendeshwa na wakafri 7 waliofunzwa nchini Lybia, nchi anayoongoza mrugaruga Kadhafi, wayanguyangu hao 7 walionyeshwa kwa wapashaji wa habari wa Taifa na wa nchi za kigeni. Bila kusahau wale wa ubalozi wa nchi rafiki, mjini Kinshasa.

Mambo hayo yalifanyika kunako wizara ya mambo ya nje na uhusiano baina ya mataifa.

Ni hivi wakafri nao 7 walionyeshwa kiserikali na katibu wa wizara ya Uhaki, mwananchi Phanzu.

Majina yao ni : Kikosi Kiboko, Simba Mutabe, walioshikwa mateka mnamo tarehe 18 Mayi 1985, baada ya mharamia Kadhafi kutusi nchi yetu Zaïre na viongozi wake mjini Bujumbura, nchini Burundi. Hawa walishikwa katika mkoa wa Luvungi hapo Rugombo kunako mpaka wa Burundi. Wahuni hao walikuwa na vifaa vya kivita kama vile mabomu ya kubomoa kituo cha "Sauti ya Zaïre", "Bralima", "mahoteli na vyumba kazaa vya utalii mjini Bukavu.

Wengine warugaruga walishikwa mnamo tarehe 5 Juni 1985 kunako mipaka ya Zaïre na Burundi. Mambo hayo yote yalihadisiwa na mharamia Kikosi Kaboko.

Ilijulishwa kuwa walivutwa nchini Tanzania Burundi wakipitia Ulaya hadi nchini Lybia ambako walifunzwa kiaskari na ginsi ya kutia vitisho. Majifunzo yao yallifanyika mijini Tripolia na Bengazia nchini Lybia. Lakini yajulishwa pia kama hayo yalikuwa machache tu juu ya mpango wa kanali Kadhafi kwa kutia fujo nchini Zaïre.

BISIMWA L.-B. Tserou.

Je umesikia ...?

KUWA wafanyabyashara wa pale Uvira watetemeka siku hizi ?

16 kati yao washtakiwa na ofisi ya kuchungua magendo mipakani (OFIDA). Jamaa hao walazimishwa kulipa kati ya zaire milioni 2 hadi 7. Hali hiyo iliwatia uwasiwasi mpaka wakachukua hatua ya kufika hapa mjini Bukavu kusudi ya kumshtaki uwakili uliotoka Kinshasa kwenyi makao ya prezidenti wa chama jimboni aliye pia liwali wa jimbo la Kivu. Na hivi wakiwa na matumaini ya kuwa watapata jawabu (solutions).

Wasahau kuwa sheria ni kama kisu ambacho Warega wazoea kuita "mbosho"

KWAMBA kupana kituliro kuna mipaka ?

Katika siku zilizopita, kiongozi wa shirika moja hapa mjini Bukavu alijaribu kuwapatia rushwa (kituliro) wanamemba wa uwakili wa wizara ya kutoza ushuru (contributions) kutoka Kinshasa. Pahali pa zaire milioni 44 alizopashwa kulipa serikali, jamaa huyo aliwaelezea kuwa atawatolea zaire milioni 4.

Ila mambo hayakuendeka kwani hawakusikilizana juu ya krtuliro. Maneno hayo yapatikana kwa sasa katika mikono ya liwali wa jimbo.

Ni nani atakayeshinda ?

Michezo

Bukavu - Dawa/Pharmakina

Bashizi kanena : "Mwaka huu hatutaki mzaa"

Ni siku ya tatu tarehe 19, baada ya kusakanya timu la Zaïre-bank bao moja kwa bila siku ya Mungu tarehe 16 Juni, katika pambano la kwanza, katika mchezo wa marudiano jeshi la Zaïre-bank liliona nyota mbele ya lenzie la Bukavu Dawa baada ya kutoka sare moja kwa moja (1-1). Kutokana na mchezo huo, timu la Pharmakina lajikamilisha kunako mapambano yafatayo siku za usoni.

Na siku ya Mungu, tarehe 9 Juni 1985, wanamemba wa timu shujaa la Bukavu-Dawa/Pharmakina mjini Bukavu walikutana kunako chumba cha Chama (Cercle du Parti) mtaani Kadutu ili kuchungua kwa karibu matatizo mbalimbali yanayoweza kumsonga na hivi kumfungia njia hadi kujinyakulia taji la timu bingwa la mji wa Bukavu kwanza na la Taifa siku za usoni.

Prezidenti wa timu hilo, mwananchi Bashizi Zahinda anena kuwa mwaka huu hawataki mzaa ingawa watu kazaa hujitatanua kuleta mzozo katika timu. Ni hivi baada ya kuilaza matimu kazaa wa kazaa hasa lile la Zaïre-bank linalojikweza kwenyi nafasi ya kwanza na lile la Mayi-Moto, jeshi la Bukavu - Dawa lakania kuyanywesha mengine maji na uma katika michezo ifuatayo hasa katika kipindi cha marudiano.

Isiwako tu mapambano ya kawaida ya kupigania ubingwa wa mji wa Bukavu bali pia ule wa "Challenge Papa Kalala".

BISIMWA L.-B. Tserou